

# Usaidizi wa Mazishi wa Virusi vya korona (COVID-19)

Maradhi tandavu ya COVID-19 yameleta majonzi kupita kiasi kwa familia nyingi. Kwenye FEMA, ari yetu ni kuwasaidia watu kabla, wakati na baada ya maafa. Tumejitolea kusaidia kurahisisha uzito na shinikizo kiasi la kifedha linalosababishwa na virusi.

**FEMA inatoa usaidizi wa kifedha kwa gharama za mazishi zinazohusu COVID-19 zilizotozwa baada ya Januari 20, 2020.**



## Ili kustahiki usaidizi wa mazishi, ni lazima ukidhi masharti haya:

- Kifo ni lazima kiwe kimetokea nchini Marekani, ikiwemo mamlaka za Marekani, na Wilaya ya Columbia.
- Cheti cha kifo ni lazima kiashirie kuwa kifo
- kilihusishwa au kusababishwa na COVID-19.
- Mwasilishaji ombi ni lazima awe mwananchi wa Marekani, raia asiyekuwa mwananchi au mgeni anayestahiki ambaye alihimili gharama za mazishi baada ya Januari 20, 2020.
- Hakuna sharti la mtu aliyefariki kuwa mwananchi wa Marekani, raia asiyekuwa mwananchi au mgeni anayestahiki.

## Gharama zipi zitastahiki fidia?

Mifano ya gharama zinazostahiki za huduma za mazishi na kuzika au kuchoma maiti zinaweza kujumuisha, lakini haziwekewi kikomo kwa:

- Usafiri kwa hadi watu wawili ili kumtambua mtu aliyefariki
- Uhamishaji wa mwili, sanduku la maiti au chungu cha majivu
- Ardhi ya kuzika au chumba cha kuchoma maiti
- Kialamisha au jiwe la sehemu ya kuzikwa maiti
- Huduma za askofu au msimamizi wa taratibu
- Kupanga shughuli ya mazishi
- Matumizi ya waajiriwa na zana za nyumba ya mazishi
- Gharama za kuzika au kuchoma maiti
- Gharama zinazohusishwa na kuzalisha vyeti kadhaa vya kifo

## Ninahitaji kuipatia FEMA maelezo gani?

Tafadhali kuwa na maelezo yafuatayo kabla ya kuwasiliana na FEMA ili kuwasilisha ombi:

- Jina lako, nambari ya usalama wa kijamii, tarehe ya kuzaliwa, anwani ya barua na nambari za simu za wawasiliani.
- Jina, nambari ya usalama wa kijamii na tarehe ya kuzaliwa ya kila mtu aliyefariki.
- Eneo au anwani ambapo mtu aliyefariki alikufa.
- Hati na risiti kwa usaidizi wowote ambao tayari umepokewa kutoka kwenye vyanzo vingine, ikiwemo kuzika au michango, bima ya mazishi, mawakala ya kujitolea, mipango mengine ya serikali au mashirika yasiyokuwa ya faida.
- Ikiwa wewe na mtu mwingine nyote mlihimili gharama za mazishi za mtu sawia aliyefariki, pia unaweza kumweka mtu huyo awe mwasilishaji ombi mwenza – ikiwemo jina lake, nambari ya usalama wa kijamii na tarehe ya kuzaliwa kwenye ombi.

## NINAWASILISHA OMBI VIPI ILI KUPATA USAIDIZI HUU?

**Pigia Simu COVID-19 ya FEMA  
Nambari ya Msaada ya Usaidizi  
wa Mazishi kwa nambari  
1-844-684-6333  
(TTY: 800-462-7585)  
kuanzia 9 AM hadi 9 PM ET,  
Jumatatu – Ijumaa na kuanza  
mchakato wa ombi.**

**Ili kupokea huduma ya upesi  
zaidi baada ya ombi lako,  
unaweza kuanza kuwasilisha  
hati mtandaoni kupitia  
[Disasterassistance.gov](https://disasterassistance.gov)  
kwa faksi 855-261-3452.  
Hati pia zinaweza kutumwa  
kwa barua hadi:**

COVID-19 Funeral Assistance  
P.O. Box 10001  
Hyattsville, MD 20782

## MASWALI YANAYOLIZWA SANA

**Pia unaweza kutuzuru  
mtandaoni hapo  
[FEMA.gov/funeral-assistance/faq](https://fema.gov/funeral-assistance/faq).  
Maelezo yanapewa kwa lugha  
kadhaa kwa simu na tovuti.**



**FEMA**